23. Uwasilishaji wa nyaraka zingine za bajeti mbele ya Bunge.
24. Kuidhinishwa kwa bajeti ya taifa na Bunge.
25. Matumizi ya Serikali yaliyoidhinishwa.
26. Wakati ambapo Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali haijaanza kutumika.
27. Mwisho wa Matumizi ya fedha iliyoidhinisha kwa mwaka wa fedha.
28. Muda wa matumizi na kibali.
29. Kuwasilisha viashiria vya Sera ya Bajeti.
30. Kuwasilisha Muswada wa Fedha.
31. Kuzuia idhini.
32. Serikali kukiuka malengo ya kibajeti.
33. Vyanzo vya Mfuko wa Dharura.
34. Waziri kusimamia Mfuko wa Dharura.
35. Matumizi kutoka Mfuko wa Dharura.
36. Bunge kuidhinishwa kwa fedha zilizotumika kutoka Mfuko wa Dharura.
37. Taarifa za fedha kuhusu Mfuko wa Dharura.
38. Mapato na uwekezaji.
39. Uhamisho wa fedha.
40. Mapato ya ziada.
41. Kuwasilisha bajeti ya nyongeza.

SEHEMU YA TANO
UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA WA BAJETI

42. Mamlaka ya Matumizi.
43. Idhini ya kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu.
44. Utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu.
45. Kibali cha Mhasibu Mkuu.
46. Dhana ya miadi.
47. Miadi ya miaka mingi.
48. Mfumo wa udhibiti wa miadi.
49. Mikataba ya Miradi ya Maendeleo.
50. Taarifa za ndani ya mwaka.
51. Taarifa za utekelezaji.
52. Taarifa za Serikali za robo mwaka.

SEHEMU YA SITA
USIMAMIZI WA MAPATO

53. Msingi ya Usimamizi wa Mapato.
54. Majukumu ya Ukusanyaji Mapato na Usimamizi.

SEHEMU YA SABA
USIMAMIZI WA VIFUNGU VIDOGO NA SERIKALI NA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

55. Usimamizi wa kibajeti na kifedha za Serikali za Mitaa.
56. Usimamizi wa kibajeti na kifedha na wa asasi nyingine za Serikali.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA JUMLA

57. Kanuni na maelekezo.
58. Kuongeza Kipindi cha muda uliowekwa.
59. Uwajibishaji wa Mamlaka iliyoshindwa kutekeleza matakwa ya Sheria.
60. Hatua za urekebishaji dhidi ya Serikali na taasisi za umma.
61. Kinga kwa maafisa wa umma.
62. Masharti ya kuwa na mamlaka ya juu.
63. Masharti ya mpito.

## TAARIFA

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni unachapishwa kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma ukiwa pamoja na maelezo yake ya madhumuni na sababu.

Dar es salaam,
30 Oktoba, 2014

**OMBENI Y. SEFUE**
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

## MUSWADA
*wa*

Sheria kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia mchakato wa bajeti ya taifa, kuweka misingi ya sera ya bajeti, Mipango na Miongozo ya Bajeti, mamlaka ya Bunge kuhusiana na bajeti; kuainisha mamlaka na majukumu ya Waziri, Katibu Mkuu, Tume ya Mipango na Kamishna wa Bajeti kuhusiana na uandaaji na upitishwaji wa bajeti ya taifa, matumizi na utoaji fedha; kuainisha uanzishaji na usimamizi wa Mfuko wa Dharura, utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu, usimamizi wa mapato, usimamizi wa Serikali na taasisi za umma na kwa ajili ya kuainisha masuala mengine yanayohusiana na hayo.

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano.

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Bajeti ya mwaka, 2014 na itaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2015.

Matumizi

**2.** Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri

**3.** Katika sheria hii, isipokuwa pale ambapo muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura 348

"Mhasibu Mkuu wa Serikali"atakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Fedha ya Umma;

Sura 348

"Afisa Masuuli" atakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Fedha ya Umma;

"Sheria ya kuidhinisha matumizi ya fedha" maana yake ni sheria inayohusu matumizi ya fedha za umma kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya usambazaji wa huduma ndani ya mwaka wa fedha;

"bajeti" maana yake ni makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka mzima na yanajumuisha misaada kwa Serikali za mitaa ambayo imewasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuidhinishwa;

"mzunguko wa bajeti" maana yake matukio yanayofuatana yanayoonyesha muda wa utakaotumika katika maandalizi ya bajeti kuanzia uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, usimamiaji na utoaji taarifa;

"taarifa ya utekelezaji" maana yake ni moja kati ya taarifa nyingi ambazo zinawasilishwa Bungeni na waziri chini ya kifungu cha 51;

"mfuko wa dharura" maana kama ilivyotafsiriwa katika Katiba;

Sura 2 "Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"wakala wa asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti" maana yake idara zinazoendeshwa nje ya bajeti ya Serikali;

"mwaka wa fedha" maana yeke ni, kuhusiana na:

(a) Serikali kuu, kipindi cha miezi kumi na mbili kinachoishia tarehe 30 Juni, ya kila mwaka;

(b) Serikali za mitaa, ili iliyotafsiriwa kwenye Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa;

(c) mamlaka ya umma au taasisi zingine, kipindi kilichobainishwa ndani ya sheria husika au nyaraka zinazohusiana na mamlaka hiyo au taasisi au kipindi kitakachowekwa na mamlaka yenye mamlaka kwa mamlaka hiyo ya umma au taasisi;

"Serikali" maana yake ni Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretariati za mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya fedha;

"miswada ya fedha" maana yake ni Muswada wa Fedha, muswada wa matumizi au muswada mwingine wowote ambao unaweka utaratibu wa masuala ya kifedha;

"mwaka ujao wa fedha" maana yake ni kipindi kinachoanzia tarehe 1 Julai ya mwaka mwingine na kuishia tarehe 30 Juni, ya mwaka unaofuata;

"Mlipaji Mkuu wa Serikali" maana yake afisa aliyepewa mamlaka ya kusimamia fedha za umma kwa mafiasa

masuuli na ambaye kwa mamlaka yake atazingatia maelekezo ya Waziri, atasimamia fedha za umma katika Wizara na Idara za Serikali na kufanya kazi nyinginezo kama itakavyoainishwa katika kanuni.

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu Hazina;

"taasisi ya umma" maana yake ni wakala, mamlaka na taasisi zote za umma ikijumuisha mashirika ya umma;

"fedha za umma" zinajumuisha:

(a) mapato ya umma ya Jamhuri ya Muungano;

(b) amana au fedha yoyote ambayo imetunzwa kwa muda au vinginevyo na afisa kwa nafasi yake ya kiofisi, aidha peke yake au kwa pamoja na mtu mwingine, awe afisa au la;

"jumuiya za kiuchumi za kikanda" zinajumuisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Soko la pamoja la Afrika Mashariki na Kusini wa Afrika na Jumuiya nyinginezo za kiuchumi;

"sheria ya matumizi ya ziada" maana yake ni sheria yoyote ambayo lengo lake ni kuongeza matumizi kwenye matumizi ambayo yalishaidhinishwa kwenye sheria ya matumizi;

Sura 370

"Msajili wa Hazina" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Msajili wa Hazina (kazi na mamlaka).

## SEHEMU YA PILI
## MUUNDO WA MFUMO WA UCHUMI JUMLA NA BAJETI

Misingi ya sera za bajeti

4.-(1) Serikali na taasisi za umma, katika malengo ya sera zao, itazingatia misingi ya usimamizi mzuri wa fedha.

(2) Misingi ya usimamizi mzuri wa fedha itajumuisha-

(a) sera ya kukopa ambayo inahakikisha umma kwamba madeni yake yanahimilika;

(b) sera za bajeti ambazo zitasaidia kufanikisha na kudumisha kiwango maalum cha tahadhari ili kuwa katika hali nzuri ya kibajeti siku za usoni;

(c) kupunguza athari za kibajeti kwa nchi kwa mujibu wa dhamana za mikopo, wajibu katika pensheni na madeni yasiyolipwa;

(d) sera ya mishahara inayohimilika, kuvutia, inayoendana na ukubwa wa uchumi, na inayohakikisha kuwepo kwa wafanyakazi wenye tija;

(e) sera izinazohakikisha kuwepo kwa mabadiliko ya wastani katika kiwango na uhakika wa viwango

vya kodi;

(f) mfumo na bajeti ya Taifa yenye kuzingatia uwazi, uwajibikaji na usimamizi mzuri wa uchumi ma sekta binafsi;

(g) vipaumbele katika matumizi yenye tija badala ya matumizi yasiyo na tija katika mgawanyo wa rasilimali na

(h) kuzingatia dhana ya mgawanyo wa mamlaka kwa kuhakikisha kwamba Bunge linashirikishwa tu katika usimamizi wa rasilimali za umma kama ilivyobainishwa na Katiba na sheria nyingine yoyote.

(3) Waziri atahakikisha kwamba misingi ya usimamizi mzuri wa fedha inazingatiwa wakati wa kuandaa na kutoa taarifa Bungeni juu ya mambo yote yanayotakiwa kutolewa taarifa chini ya Sheria hii.

(4) Serikali inaweza kutozingatia misingi ya usimamizi mzuri wa fedha kama Waziri-

(a) ataeleza sababu za kutozingatia misingi hiyo ikijumuisha mpango wa utekelezaji na kipindi ambacho Serikali itakuwa haizingatii misingi ya usimamizi mzuri wa fedha; na

(b) atawasilisha sababu, mpango wa utekelezaji na kipindi cha kutokuzingatia misingi hiyo mbele ya Bunge kwa ajili ya kupitishwa kabla utekelezaji wa sera ya usimamizi wa fedha.

(5) Ukiukwaji wa malengo ya kibajeti utapimwa na kutolewa maelezo katika Mwongozo wa uandaaji Mpango na Bajeti wa mwaka unaofuata.

Malengo ya sera za bajeti

**5.** Mpango na Bajeti utabainisha malengo ya bajeti kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo-

(a) kuhamasisha uhimilivu wa uhakika wa uchumi jumla na ukuaji wa uchumi shirikishi usiokuwa na mfumuko wa bei;

(b) kuanzisha na kuweka mfumo himilivu wa kibajeti na athari ndogo za deni la Taifa;

(c) kuweka wa ukomo wa kibajeti utakaozuia mapungufu katika masuala ya fedha ikiwemo mikopo;

(d) kuweka kiwango cha kutosha cha akiba ya Taifa kuwezesha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi; na

(e) kuwa na uhimilivu na uhakika katika masuala ya fedha.

Matarajio ya uchumi jumla na bajeti

6. Programu bajeti na uudaji wa uchumi jumla unaotumika kwa ajili ya sehemu ya mwaka wa fedha kama nyenzo ya uandaaji wa mfumo wa uchumi jula pamoja na mpango na bajeti utahusisha-

(a) kutathmini mwenendo wa uchumi wa dunia na athari zake kwenye uchumi wan chi;
(b) kuandaa makisio ya muda wa kati ya uchumi jumla na matarajio ya mwaka ujao wa fedha;
(c) kuandaa uchumi jumla wa muda wa kati utakaotumika kwa ajili ya kuandaa mpango na bajeti;
(d) kuandaa mahitaji yanaohusu uchumi jumla na matarajio ya bajeti kwenye nayraka za mpango na bajeti ya taifa; na
(e) kubainisha majuku ya waziri kutoa matarajio ya uchumi jumla na bajeti kwa kuzingatia muda wa kati.

Utaratibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa

7.-(1) Serikali na Taasisi za Umma zitaandaa bajeti zao za mwaka kwa kuzingatia mpango wa muda wa kati na muda mrefu.

(2) Bajeti itakayoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) itajielekeza kwenye kutekeleza mpango wa maendeleo wa taifa.

(3) Wakati wa kuandaa bajeti chini ya kifungu hiki, Serikali na Taasisi za Umma hazotjumuishwa kwenye bajeti zao, mradi wowote ambao haukuorodheshwa kwenye mpango wa maende wa Taifa.

(4) Serikali na Taasisi za Umma zitakahkikisha kwamba-

(a) mipango ya maendelo iliyoidhinishwa ndiyo pekee inatekelezwa;
(b) mahitaji ya kifedha ya mpango wa maendelo wa taifa yanarandana na kiwango cha ukomo kilichonyeshwa kwenye mpango wa bajeti iliyoelezwa kwenye sheria hii;
(c) miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa vipaumbele;
(d) utaratibu wa kutekeleza bajeti ya maendeleo na matumizi, unaanzishwa;
(e) utaratibu wa kupitia upya mradi wowote mpya wa maendeleo kabla ya kuanza utekelezaji wake, unaanzishwa;
(f) miradi ya maendeleo inaidhinishwa na Tume ya

Mipgango kabla haijajumuishwa kwenye bajeti;

(g) ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuchangia na kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kupitia ubia baina ya sekta binafsi na umma;

(h) vigezo vya juibua vyanzo vya mapato ya serikali za mitaa, vinawekwa;

(i) upangaji wa madaraja ya serikali za mitaa kwa jaili ya mipango na ugawaji fedha, unafanyika;

(j) muda kwa ajili ya kukandaa na kusambaza mpango na bajeti unawekwa; na

(k) vigezo ambavyo kwayo fedha itagawiwa kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya maendeleo, vinawekwa.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI WA MCHAKATO WA BAJETI

Majukumu ya Bunge

8.-(1) Bunge litakuwa na majukumu yafuatayo-

(a) kujielekeza kwa makadirio ya awali na mpango wa uchumi jumla na programs;

(b) kujadili na kupitia upya mpango na makisio ya bajeti;

(c) kusimamia masuala yote ya kibajeti yanayoingia kwenye mamlaka ya Bunge;

(d) kuchambua taarifa za kifedha na nyaraka zingine zilizowasilishwa kwake na kutoa maoni kwa Serikali kuhusu uboreshaji wa usimamizi wa fedha za umma;

(e) kushauri Serikali kuhusu Sheria ya Fedha baada ya kuzingatia maoni ya Waziri;

(f) kutoa ushauri wa jumla kuhusu mwelekeo wa bajeti kwa usuluhishi wake; na

(g) kufanya shughuli yoyote inayohusiana na bajeti ambayo sheria yoyote itaitaka kuifanya.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake, Bunge litazingatia misingi ya usimamizi mzuri wa fedha katika mfumo wa bajeti.

(3) Waziri ataainisha utaratibu ambao Bunge litawasilisha maoni na mapendekezo ambayo yanaweza kuzingatiwa katika uandaaji wa makadirio ya bajeti ya Taifa.

Mamlaka na kazi za waziri

9.-(1) Waziri katika kila mwaka wa fedha ataandaa na kuwasilisha Bungeni-

(a) makadirio ya mapato; na

(b) makadirio ya matumizi na mahitaji ya fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa mwaka huo.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Waziri atakuwa na wajibu wa-

(a) kuandaa sera ya uchumi jumla na mpango wa matumizi wa bajeti wa muda wa kati;

(b) kudhibiti na kusimamia uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa bajeti, ikijumuisha marekebisho yoyote kwenye bajeti;

(c) kuhakikisha kuwa wadau wote wanashirikishwa na kufahamishwa kuhusu maamuzi ya kibajeti katika mpango wa muda wa kati ulioandaliwa na waziri chini ya aya (a);

(d) kutangaza kwa njia zingine zinazofaa, maendeleo ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo mwaka;

(e) kusimamia na kudhibiti fedha za Serikali, michakato ya kibenki na malipo, matarajio ya upatikanaji wa fedha, deni la umma na mali na madeni ya Serikali;

(f) kutangaza na kutekeleza uwazi na usimamizi yakinifu wa mapato, matumizi, mali na madeni ya Serikali.

(3) Waziri kwa kutumia kanuni-

(a) ataainisha utaratibu wa jinsi, wakati na mahali ambapo umma utashirikishwa katika maandalizi ya bajeti kwa ngazi ya kitaifa; na

(b) Kamishna wa Bajeti na Mkaguzi Mkuu wa Ndani watatoa utaratibu wa usimamizi wa bajeti kwa kuhakikisha ushiriki binafsi wa maafisa masuuli katika kazi za kamati za bajeti.

Majukumu ya Waziri anayeshughulikia masuala ya Mpango

**10.** Waziri anayeshughulikia masuala ya Mipango atakuwa na jukumu la-

(a) kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa;

(b) atawasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuidhinishwa;

(c) atawasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa ulioidhinishwa kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge;

(d) ataratibu utekelezaji wa Mpango wa

Maendeleo wa Taifa; na

(e) kuwasilisha Bunge taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa.

Mamlaka na kazi za Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali

**11.**-(1) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii na sheria ndogo zitakazotengenezwa chini ya sheria hii atawajibika kwa Waziri.

(2) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali atahakikisha kwamba-

(a) maandalizi ya makadirio ya matumizi kwa mwaka yanafanyika kwa umakini na wakati kwa ajili ya kuzingatiwa na kuidhinishwa na Waziri kwa kuzingatia idhini la Baraza la Mawaziri kabla ya kuwasilishwa bungeni;

(b) makadirio ya mwaka ya matumizi yanaandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya jumla au mahsusi ya waziri inayoonyesha, kadiri iwezekanayavyo, thamani ya fedha na matumizi bora ya rasilimali za Serikali;

(c) mifuko maalum iliyopo na inayokusudiwa kuanzishwa inapitiwa; na

(d) mfumo utakaowezesha mifuko maalum kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, unaanzishwa.

(3) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, kwa kuzingatia maelekezo ya waziri atadhibiti utoaji wa fedha za umma kwa Serikali na taasisi zingine za umma na atafanya kazi zingine zozote zitakazo bainishwa na waziri.

(4) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali anaweza kuomba taarifa ambayo ni muhimu kwa jili ya kuandaa taarifa yoyote chini ya sheria hii.

(5) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (4) yatakuwa ya maandishi yanayobainisha masharti na tarehe pamoja na muonekano wa taarifa itakayotolewa na taasisi ya umma ambayo itatakiwa kutii ombi.

(6) Afisa yeyote wa umma ambaye, bila sababu madhubuti, atashindwa kutoa taarifa iliyoombwa chini ya kifungu hiki anafanya kosa la kinidhamu na atachukuliwa hatua za kinidhamu ambazi zitalingana na mazingira ya kosa.

(7) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa madhumuni ya kuhakikisha matumizi bora ya fedha za umma kwa taasisi za umma itafanya marejeo ya

mapato na matumizi ya taasisi za umma.

(8) Katika kufanya marejeo hayo mara kwa mara Katibu Mkuu anaweza kuamuru kiasi chochote cha fedha kuingizwa katika bajeti ya taifa.

(9) Waziri anaweza, kupitia kanuni zilizotangazwa kwenye gazeti la Serikali, kubainisha utaratibu wa kufanya marejeo hayo ya mapato na matumizi ya taasisi za umma.

Mamlaka na kazi ya Tume ya Mipango.

**12.** Mamlaka na kazi za Tume ya Mipango zitakuwa-

(a) kutathmini hali ya raslimali za taifa kwa maendeleo na kuishauri Serikali juu ya matumizi sahihi ya raslimali hizo;

(b) kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Serikali kuhusu mipango na usimamizi wa uchumi;

(c) kuchambua miradi ya kimaendeleo ili kujumuishwa kwenye bajeti ya maendeleo; na

(d) kutoa mwongozo wa uandaaji wa Mpango wa Taifa na kufutilia mchakato wa maandalizi wa mipango ya mwaka wa muda mfupi, kati na mrefu.

Kamishna wa Bajeti

**13.**-(1) Kutakuwepo na Kamishna wa Bajeti.

(2) Kamishna wa Bajeti kwa maelekezo ya Katibu Mkuu atawajibika kuandaa, kutekeleza, kusimamia, kutathmini na kutoa taarifa juu ya bajeti.

(3) kamishna wa Bajeti katika kutekeleza majukumu yake atawajibika kwa Katibu Mkuu.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, Kamishna wa Bajeti atakuwa na jukumu la-

(a) kupitia sera za bajeti na kutoa mwongozo kwenye eneo hilo;

(b) kuchambua mafungu tofauti ya bajeti wakati wa mchakato wa kuandaa mafungu hayo;

(c) kusimamia bajeti ya Serikali na taasisi za umma;

(d) kuandaa taarifa za uhamisho wa fedha;

(e) kusimamia, kutathmini na kutoa taarifa kuhusu bajeti ya Serikali;

(f) kusimamia na kujumuisha mpango wa mtiririko wa fedha wenye kuzingatia utekelezaji na utoaji taarifa; na

(g) kutoa ushauri kuhusu miadi ya Serikali yenye kuhitaji rasilimali fedha na taratibu za

kibajeti.

Kamati ya kitaifa ya mpango na bajeti

**14.**-(1) Kutakuwepo na Kamati ya Kitaifa ya mpango wa bajeti.

(2) Muundo wa kamati ya kitaifa ya mpango wa bejeti utaainishwa na Waziri kupitia kanuni.

(3) Kamati ya kitaifa ya mpango na uchumi itakuwa na jukumu la kuishauri Serikali katika kuandaa Bajeti ya nchi.

(4) Mamlaka na kazi ya kamati ya kitaifa ya mpango na Bajeti yatakuwa:

(a) kuandaa mpango na bajeti kwa mujibu wa sheria hii;

(b) kuomba taarifa kwa maandishi kutoka Serikalini na taasisi za umma ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuandaa Mipango na Miongozo ya Bajeti;

Kamishna wa Uchambuzi wa Sera

**15.**-(1) Kutakuwa na Kamishna wa Uchambuzi wa Sera.

(2) katika kutekeleza majukumu yake Kamishna wa Uchambuzi wa Sera atakuwajibika kwa Katibu Mkuu.

(3) majukumu ya Kamishna wa Uchambuzi wa Sera yatakuwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu wa kisera kuhusiana na-

(a) masuala ya kisera kuhusu bajeti, ukusanyaji wa mapato, mgawanyo wa matumizi, vyanzo vya fedha na mahusiano ya kiuchumi ya kikanda na kimataifa; na

(b) masuala ya uchumi jumla kuhusu utungaji wa sera na utekelezaji, usimamizi wa kanzidata na utoaji wa taarifa wa vipindi.

Mamlaka na kazi ya Msajili wa Hazina

16. Msajili wa Hazina atakuwa na mamlaka na kazi ya-

(a) kupitia na kupendekeza au kupitisha mikakati na mipango ya mwaka ya taasisi za umma ambazo ziko chini ya usimamizi wa Msajili wa Hazina kabla ya kuiingiza kwenye mpango wa Maendeleo ya Taifa;
(b) kusimamia mifuko ya uwekezaji wa taasisi za umma;
(c) kufuatilia na kuhakikisha kwamba ziada, michango na gawio kutoka taasisi za umma zinalipwa kwa wakati;
(d) kuelekeza au kupitisha, matumizi au marekebisho ya Kanuni za fedha ili kuhakikisha mapato na matumizi ya taasisi za umma;
(e) kusimamia mitaji, ruzuku, fedha za mitaji, akiba au mapato yaliyosalia, yaliyolipwa na shirika na uwekezaji mwingine wa umma;
(f) kuchambua na kuidhinisha muundo wa taasisi,muundo wa mishahara,**kada za utumishi** katika taasisi za umma;
(g) kusimamia fedha zilizopokelewa kutokana na ubinafsishaji wa taasisi za umma, mali na hisa;
(h) kufanya mapitio na kusaini mikataba ya utekelezaji ya mashirika ya umma yenye lengo y kuboresha mapato; na

Mamlaka na kazi ya Maafisa Masuuli

17.(1)-Mamlaka na kazi za Maafisa Masuuli zitakuwa ni kuhakikisha kwamba-

(a) mafungu ya bajeti na taasisi za umma zinaandaliwa kwa mujibu wa Miongozo na Miongozo ya Bajeti;
(b) fedha za umma na rasilimali za umma zinalindwa na kusimamiwa ipasavyo; na
(c) kuna mpangilio mzuri wa kuwezesha kukusanya mapato kutoka kwa umma.

(2) Maafisa Masuuli wa Wizara na taasisi za umma wataanzisha kamati za bajeti ambazo muundo wake utaainishwa katika kanuni.

## SEHEMU YA NNE
## UANDAAJI NA UIDHINISHWAJI WA BAJETI

Hatua za uandaaji wa bajeti

**18.**-(1) Matayarisho ya Bajeti kwa kila mwaka wa fedha yatahusisha hatua zifuatazo-

(a) majumuisho ya mchakato wa mipango ya maendeleo ambayo itakuwa ile mipango ya muda mrefu na muda wa kati;

(b) mipango na maamuzi ya sera za kifedha na kiuchumi pamoja na vipaumbele vya ngazi ya kitaifa kwa muda wa kati;

(c) Baraza la Mawaziri kuidhinisha Mwongozo wa Mpango wa Bajeti;

(d) Bunge kuidhinisha Mwongozo wa Bajeti na Mpango kama msingi wa maamuzi ya baadaye;

(e) Baraza la Mawaziri kuidhinisha hatua na vyanzo vya mapato;

(f) Bunge kuidhinisha hatua na vyanzo vya mapato;

(g) kuwasilisha makadirio ya bajeti Bungeni kwa ajili ya kupata kibali;

(h) kuandaa Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali, Muswada wa Sheria ya Fedha na Sheria nyingine zinazohitajika kutungwa kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo ya Bajeti ya Serikali;

(i) kutunga Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali na Sheria ya Fedha;

(2) Kutakuwa na kamati ya kumshauri Waziri kuhusu vyanzo vya mapato katika mwaka wa fedha husika.

(3) Muundo wa kamati ya hiyo ya ushauri utaainishwa na Waziri katika kanuni.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa

**19.** Waziri anayeshughulikia Tume ya Mipango ataandaa na kuwasilisha Bungeni Mpango wa Maendeleo wa Taifa ambao utakuwa msingi wa uandaaji wa bajeti ya Taifa.

Mpango na Mwongozo wa Bajeti

**20.**-(1) Waziri ataandaa na kuwasilisha Bungeni Mpango na Mwongozo wa Bajeti.

(2) Mpango na Mwongozo wa Bajeti utawasilishwa Bungeni kila Februari ya kila mwaka, au

pale ambapo Bunge halitakuwepo mwezi Februari, kila wiki ya kwanza Bunge litakapokutana.

(3) Mpango na Miongozo ya Bajeti utaeleza kwa mapana malengo ya masula ya Uchumi Jumla ambayo yatakuwa msingi wa bajeti kwa kipindi kinachofuata mwaka wa fedha uliopo na mipango ya kati na itazingatia yafuatayo-

(a) tathimini ya mwaka wa fedha uliopo na uchumi unaotarajiwa kwa miaka ya fedha mitatu inayofuata;

(b) uchumi jumla na sera za kibajeti kwa kipindi kilichobainishwa chini ya aya (a);

(c) malengo ya mapato kwa ujumla, matumizi kwa ujumla, ukopaji wa ndani nan je kwa kipindi kinachofuata mwaka wa fedha na mipango ya kati;

(d) jumla ya rasilimali zilizogawanywa kwa ajili miradi ya kisekta au Wizara kwa kipindi kilichobainishwa chini ya aya (a) ilibainisha matokeo yanayotarajiwa kutoka kwa kila mradi kwa kipindi hicho;

(e) vigezo vilivyotumika kugawa rasilimali za umma zilizopo kwa kila mradi;

(f) makadirio ya riba na gharama za ulipaji madeni na ulipaji wa madeni kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa bajeti husika na miaka miwili ya fedha inayofuata;

(g) mapendekezo ya kugharimia mapungufu yoyote kwa mwaka wa fedha;

(h) makusudio kuhusu ukopeshaji na vitu vitakavyosababisha kuongezeka kwa deni ya Taifa kwa mwaka wa fedha;

(i) bajeti na hali halisi ya mapato kwa miaka miwili ya fedha iliyotangulia;

(j) bajeti na hali halisi ya matumizi kwa miaka miwili ya fedha iliyotangulia kwa kila fungu na Idara muhimu;

(k) makadirio ya hali ya kifedha kwa mwaka wa fedha unaohusika na bajeti na miaka miwili inayofuata;

(l) malengo ya kisera yanayosimamia maamuzi ya bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha na maeneno ya kisera ambayo Serikali itazingatia katika mwaka wa fedha.

Bajeti za taasisi za umma

**21.**-(1) Taasisi za Umma zitatakiwa kuandaa makadirio ya bajeti na kuziwasilisha kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya uchambuzi na idhini kwa mujibu wa Sheria hii na kupokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa.

(2) baada ya kupokea makadirio ya bajeti, katibu mkuu anaweza:

(a) kuidhinisha makadirio ya bajeti yakiwa na mabadiliko au bila mabadiliko;

(b) kukataa makadirio ya bajeti na kutoa sababu za kukataa;

(3) Katibu Mkuu anaweza kufanya mabadaliko au kukataa makadirio ya bajeti kwa misingi ya sababu mahsusi zilizotajwa kama zinazoainishwa-

(a) makadirio hayaangukii katika majukumu ya msingi ya taasisi za umma husika;

(b) makadirio hayo ni ya juu zaidi na hayalingani na mahitaji halisi ya utoaji au upokeaji wa huduma katika soko au

(c) hayaendani na hatua za kubana matumizi zilizoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa.

(4) Katibu Mkuu anaweza, kuamuru mapato yaziada ya bajeti yaliyokusanywa na taasisi za umma kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu .

Uwasilishaji wa makadilio ya bajeti

**22.**-(1) Waziri atatakiwa, katika kipindi kilichowekwa na kubainishwa katika kifungu hiki, kuwasilisha kwa Baraza la Mawaziri kupata kibali-

(a) makadirio ya bajeti na nyaraka nyinginezo zinazozingatiwa katika bajeti; na

(b) rasimu ya miswada ya fedha inayotakiwa kutekeleza bajeti.

(2) Pale ambapo Baraza la mawaziri litakapokuwa limetoa kibali kwa makadirio ya bajeti kwa mujibu wa kifungu kidogo (1), Mawaziri wote watatakiwa kuwa na jukumu la;

(a) kuzingatia, kufuata na kusimamia makadilio ya bajeti;

(b) kusimamia utekelezaji wa makadirio ya bajeti

(3) Waziri atatakiwa kufikia tarehe 30 Aprili kila mwaka, kuwasilisha Bungeni nyaraka zifuatazo-

(a) makadirio ya bajeti;

(b) nyaraka zinazohusiana na makadirio ya bajeti kwa ajili ya utekeleza wa bajeti.

(4) Waziri atatakiwa kuhakikisha maandalizi ya bajeti yanafanyika kwa kuzingatia na ndani ya muda ulioainishwa kuwezesha washiriki wa maandalizi wanazingatia matakwa ya Katiba na Sheria hii.

(5) Waziri baada ya kuwasilisha Bungeni Makadirio ya bajeti na nyaraka zinazohusiana na makadirio ya bajeti kama inavyobainishwa na Kifungu hiki, atatangaza nyaraka na kuzisambaza kwa umma.

(6) Waziri mara baada ya kupata kibali cha Bunge kuhusu makadirio ya bajeti, ataandaa na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa makadirio yaliyoidhinishwa na Bunge.

Uwasilishaji wa nyaraka zingine za bajeti mbele ya Bunge

**23.**-(1) Pamoja na nyaraka zilizowasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 22, Waziri atapaswa kuwasilisha Bungeni nyaraka za bajeti kwa kila mwaka wa fedha-

(a) muhtasari wa bajeti unaojumuisha:
  (i) muhtasari wa sera za kibajeti zinazojumuisha sera za mapato, matumizi, madeni na upungufu wa fedha;
  (ii) maelezo ya jinsi bajeti inavyohusika na misingi ya wajibu wa kibajeti na malengo ya kibajeti na
  (iii) maelezo ya Waziri kuhusu makubaliano ya Bunge kwenye Mpango na Miongozo ya bajeti ilivyoshughulikiwa;

(b) muundo wa makadirio ya bajeti yanayojumuisha:
  (i) orodha ya taasisi zote zinazopata fedha kutoka bajeti ya Serikali;
  (ii) makadirio yote ya mapato kwa wigo mkubwa wa uchumi;
  (iii) makadirio yote ya matumizi, mafungu ya miradi, ikibainisha matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo; na
  (iv) makadirio ya mapungufu ya bajeti au ongekezo kwa mwaka wa fedha na mipango ya kati na mapendekezo ya vyanzo vya fedha;

(c) taarifa kuhusu madeni yatokanayo na bajeti ya Serikali, inayojumuisha makadirio ya deni, riba na gharama zinginezo zinazotakiwa kulipwa na Serikali katika mwaka wa fedha kwa mujibu wa madeni husika;

(d) taarifa kuhusu madeni na dhamana za Serikali, yanayojumuisha makadirioya deni, riba na gharama zinginezo zinazotakiwa kulipwa na Serikali katika mwaka wa fedha kwa mujibu wa madeni husika;

(e) taarifa kuhusu malipo yatakayolipwa na gharama zitakazolipwa na Serikali ambazo hazikubainishwa katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali ambazo zinajumuisha masuala ya kikatiba na mamlaka ya Sheria kufanya malipo hayo na

(f) taarifa ya Waziri kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza mapendekezo ya Bunge kuhusu bajeti ya Serikali katika mwaka au miaka iliyopita.

(2) Waziri atatoa ufafanuzi wa taarifa zitakazowasilishwa pamoja na makadirio ya bajeti na mfumo wa uwasilishwaji utakaotumika.

Kuidhinishwa kwa Bajeti ya Taifa na Bunge

**24.**-(1) Bunge litaidhinisha ifikapo tarehe 30 Juni kila mwaka, bajeti ya Taifa pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata na kupitisha Muswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali, Muswada wa Fedha na hati nyingine za kisheria ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa bajeti ya Taifa.

(2) Bunge litaidhinisha bajeti ya Taifa ya mwaka kwa kupiga kura kwa kuita jina kwa kila mbunge.

Matumizi ya Serikali yaliyoidhinishwa

**25.**-(1) Waziri wa Fedha atahakikisha kuwa matumizi yatakayoidhinishwa katika makadirio ya bajeti katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali yanawasilishwa yakiwa-

(a) sahihi na zimezingatia masuala muhimu ya kibajeti; na

(b) yamebainisha wazi fedha zilizopo katika fungu na miradi.

(2) Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali itajumuisha-

(a) matumizi ya kawaida kwa kila mradi, ikiainisha kila matumizi husika; na

(b) matumizi ya maendeleo kwa kila mradi wa maendeleo, ikiainisha kila matumizi husika.

(3) Makadirio ya bajeti yaliyoidhinishwa na Bunge yatachukuliwa kuwa kama yameidhinishwa kwa ajili ya

matumizi ya shughuli za Serikali na Taasisi za Umma.

(4) Fedha zilizoidhinisha kwa matumizi ya Serikali na taasisi za umma, zitatumika kwa kuzingatia madhumuni yaliyoainishwa na katika kiwango kilichowekwa kwa makadirio ya Serikali na taasisi za umma.

(5) Waziri katika kipindi cha siku thelathini baada ya Bunge kuidhinisha makadirio ya bajeti, ataboresha, atachapisha na kutangaza kwa umma makadirio ya bajeti.

(6) Waziri atahakikisha na kuchukua hatua kuhakikisha makadirio yaliyoidhinishwa yametayarishwa na kutangazwa katika muundo ambao utakuwa wazi na rahisi kueleweka na kupatikana kwa umma.

Wakati ambapo Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali haijaanza kutumika

**26.**-(1) Endapo Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali haijaanza kutumika, Rais anaweza kwa kutumia Warrant iliyosainiwa na resident iliyoelekezwa kwa Waziri, akaruhusu matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuwezesha kazi za Serikali kuendelea mpaka muda wa miezi minne toka kuanza kwa mwaka wa fedha kuisha au kwa kuanza kutumika kwa Sheria hii, chochote kitakachotangulia.

(2) Kiasi kitakachoruhusiwa kutumika hakitakiwi kuzidi kiasi kilichoainishwa kwa ajili ya mapendekezo ya shughuli zilizokadiwa kwa mwaka wa fedha au moja ya tatu ya kiasi kilichoainishwa katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali.

(3) Fedha zilizotumika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) kitahesabiwa kama sehemu ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali inayohusishwa.

Mwisho wa Matumizi ya fedha iliyoidhinisha kwa mwaka wa fedha

**27.**-(1) Fedha ambazo hazijatumika kufikia mwisho wa mwaka ambazo ziliidhinishwa matumizi yake yataishia mwaka huo wa fedha.

(2) Kwa kuzingatia sheria zingine, endapo mwisho wa mwaka wa fedha taasisi za umma bado ina bakaa ya fedha zilizoidhinishwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, fedha hizo zitarudishwa kwenye Mfuko Mkuu wa hazina, taasisi ya umma itaandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Kamishna wa Bajeti.

(3) Kifungu kidogo cha (2) hakitatumika kwa fedha zilizoidhinishwa kuvuka mwaka wa fedha kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Muda wa matumizi na kibali

**28.**-(1) Matumizi yote ya fedha za umma yaliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya huduma za mwaka wa fedha na kila kibali na idhini nyingine zilizotolewa na sheria hii kuhusiana na mwaka husika, itaisha na kukoma kuwa na nguvu inapofika mwisho wa mwaka wa fedha.

(2) Fedha zote ambazo hazijatumika na ambazo zilitolewa kwenye Mfuko Mkuu zitarejeshwa kwenye Mfuko Mkuu.

Kuwasilisha viashiria vya Sera ya Bajeti

**29.**-(1) Waziri, katika kila mwaka wa fedha baada ya kupata idhini ya Baraza la Mawaziri, atatangaza kwa umma viashiria vya sera za bajeti pamoja na hatua za kukusanya mapato ya Serikali.

(2) Wakati akitoa tangazo hili, atazingatia makubalino ya kikanda na kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeingia, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Afrika Mashariki mwaka 1994 na pale ambapo mikataba hiyo inahitaji kutangazwa kwa hatua hizi katika tarehe maalum, Waziri atahakikisha hatua hizi zinatangazwa katika tarehe husika.

Kuwasilisha Muswada wa Fedha

**30.**-(1) Waziri ataandaa na kuwasilisha Bungeni, Muswada wa Fedha akiainisha hatua za kuongeza mapato ya Serikali.

(2) Katika kuwasilisha Muswada wa Fedha, Bunge litawasilisha mapendekezo yake kuhusu Muswada wa Fedha.

(3) Mapendekezo yote yatakayotolewa na Bunge au kuchukuliwa na Bunge katika masuala ya mapato yata-

(a) zingatia kwamba kiwango cha mapato kitakachokusanywa kinaendana na misingi ya bajeti iliyoidhinishwa;

(b) kuzingatia misingi ya usawa, uhakika na wepesi wa kukusanya;

(c) kuzingatia athari za mapendekezo ya mabadiliko katika mchanganuo wa kodi kwa kuzingatia kodi ya moja kwa moja na kodi inayoingizwa kwenye bidhaa;

(d) kuzingatia mwenendo wa mapato ya ndani, kanda na kimataifa;

(e) kuzingatia athari katika maendeleo, uwekezaji, kukua kwa uchumi; na

(f) kuzingatia kodi na makubaliano mengine ya viwango na majukumu ambayo Jamhuri ya Muungano imechukuwa, ikiwa ni pamoja na